# TAARIFA KWA UMMA

**Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Na Dhamana (CMSA)**

## PROGRAMU YA HATIFUNGANI YA MUDA WA KATI YA BENKI YA TCB PLC: TOLEO LA KWANZA – TCB STAWI BONDI

Benki ya TCB inatoa taarifa kwa umma kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa Programu ya Miaka Mitano ya Hatifungani yenye jumla ya Shillingi za Tanzania bilioni 150. Hali kadhalika,CMSA imeidhinisha Toleo la kwanza la Programu ya Hatifungani (TCB Stawi Bondi) lenye jumla ya Shillingi za Tanzania bilioni 50.

### TAARIFA YA HATIFUNGANI TOLEO LA KWANZA - TCB STAWI BONDI

| **Mtoaji** | TCB Bank PLC |
|---|---|
| **Fedha zilizoidhinishwa** | TSH (Shilingi za Tanzania) |
| **Jumla ya kiasi cha Programu** | TSH 150,000,000,000 (Shilingi za Tanzania Bilioni Mia Moja na Hamsini Tu) |
| **Kiasi cha Toleo la Kwanza** | TSH 50,000,000,000 (Shilingi za Tanzania Bilioni Hamsini Tu) |
| **Kiwango cha riba (Interest rate)** | 13.5% kwa mwaka inayolipwa kila robo mwaka |
| **Kiwango cha chini cha Kuwekeza** | TSH 500,000 (Shilingi za Tanzania Laki Tano Tu) katika noti za TSH 10,000 (Shilingi za Tanzania Elfu Kumi) |
| **Tarehe ya toleo** | 14 Novemba 2025 |
| **Tarehe ya Kuiva Kwa Hatifungani** | 14 Novemba 2030 |
| **Tarehe za malipo ya riba** | 14 Februari, 14 Mei, 14 Agosti na 14 Novemba kila mwaka mpaka muda wa kuiva kwa Hatifungani. |
| **Tarehe ya kuanza malipo ya riba** | 14 Novemba 2025 |
| **Muda wa Hatifungani** | Miaka 5 |
| **Kodi** | Hakuna kodi ya zuio |
| **Kuorodheshwa** | Hatifungani ya Stawi itaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |

Uwekezaji unafanyika kwa kujaza Fomu ya Maombi inayopatikana kwenye matawi ya Benki ya TCB, kwa mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam waliopewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); au kwenye tovuti ya Benki ya TCB www.tcbbank.co.tz .

Maombi yatakamilishwa kwa kufanya malipo katika akaunti ya Benki ya TCB iliyoainishwa hapa chini:

**Akaunti ya Malipo**

| | |
|---|---|
| **Stawi Bond Collection Account** | **173086000001** |

**Tarehe za Matukio Muhimu:**

| Na. | Tukio | Tarehe |
|---|---|---|
| **1.** | Tarehe ya kuidhinishwa Waraka wa Matarajio na CMSA | Ijumaa 12 Septemba 2025 |
| **2.** | Kuanza kupokea maombi ya ununuzi wa Hatifungani | Jumatano 17 Septemba 2025 |
| **3.** | Mwisho wa kupokea maombi ya ununuzi wa Hatifungani | Ijumaa 17 Oktoba 2025 |
| **4.** | Mwisho wa Kupokea Malipo ya Hatifungani | Ijumaa 17 Oktoba 2025 |
| **5.** | Mgao kwa Wawekezaji | Alhamisi 30 Oktoba 2025 |
| **6.** | Kutangazwa matokeo ya mauzo ya Hatifungani | Ijumaa 14 Novemba 2025 |
| **7.** | Taarifa ya kupata Hatifungani kwa Wawekezaji | Ijumaa 14 Novemba 2025 |
| **8.** | Kuwasilishwa kwa Rejista ya Wawekezaji CSDR | Ijumaa 14 Novemba 2025 |
| **9.** | Tarehe ya toleo | Ijumaa 14 Novemba 2025 |
| **10.** | Kuingiza CDS kwenye mfumo wa DSE | Jumatano 19 Novemba 2025 |
| **11.** | Kuorodheshwa kwa hatifungani DSE | Ijumaa 21 Novemba 2025 |
| **12.** | Kuiva kwa hatifungani | 14 Novemba 2030 |

Wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenye leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Benki ya TCB**
**Ghorofa ya 10, Millenium Towers**
**Barabara ya Bagamoyo**
**S.L.P 9300, Dar es Salaam**
**Tanzania**

**Tarehe: 15 Septemba 2025**

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa mujibu wa kanuni za Mamlaka za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.